# HONGERA KWA KUOKOKA

*Karibu Katika Familia ya Mungu.*

Shemeji **Melayeki**

**Hongera kwa Kuokoka © 2025**
**Shemeji Melayeki**

**Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.**

SIMU: +255 714 548 565
+255 763 965 297
Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*
YouTube: *Shemeji Melayeki*
Instagram: *apostle_shemeji_melayeki*
Twitter: *@melayeki*
Facebook: *Ap Shemeji Melayeki*

Kimepigwa Chapa Na:
**KLIMAX SOLUTIONS – ARUSHA**
**+255 658 288 054**
**+255 687 699 862**

# KARIBU KATIKA FAMILIA YA MUNGU

Leo hii umefanya uamuzi wa busara na uamuzi bora katika maisha yako. Umeamua kumpokea Yesu awe mwokozi wako na kukupa nafasi katika familia ya Mungu, nafasi ambayo haukuwa nayo hapo awali kwa sababu ilitakiwa wewe uamini (au kupokea zawadi hii). Wewe sasa ni mwana wa Mungu. Yohana anaandika **1 Yohana 3:1a** *[1] Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo.*

**Warumi 8:15** *[15] Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba.*

Neno **kufanywa wana** maana yake ni *kule kuonekana au kutengwa kama wana*. Hivyo, tumepokea roho ya kufanywa wana, huyu Roho hushuhudia kuwa wewe u mtoto wa Mungu, uliyezaliwa kwa mbegu isiyoharibika.

**Warumi 8:16-17** *[16] Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; [17] na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.*

**Wagalatia 4:6-7** *[6] Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. [7] Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.*

Roho wa Kristo yuko ndani yako na ndani yetu. Wewe una vinasaba vya kiroho ambayo ni Roho wa Mungu au Roho wa Kristo (mwana).

Ni katika kufanyika kwako mwana wa Mungu umerithi kila kitu chema kilicho ndani ya Kristo.

**2 Wakorinto 6:18** *[18] Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike,*
Unajivunia Mungu kuwa Baba yako.

**Wagalatia 3:26** *[26] Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.*

Ulipomwamini Yesu Kristo papo hapo ulifanyika mwana wa Mungu. Wewe ni uzao wake. Kwa hiyo Yesu alikufa kwa

ajili ya dhambi zako. Akafufuka kukutangazia ushindi kwamba wewe uko huru mbali na hatia zote. Na hii ndiyo pendo kuu kwamba wewe uliyekuwa wa kukataliwa sasa umesogezwa karibu na kufanywa mwana katika familia yake.

## KAZI YAKO NI KUAMINI TU

Biblia inaweka wazi kuwa unafanyika mwana wa Mungu kwa kumwamini Yesu, angalia **Yohana 1:12** *Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake*. **Matendo 10:43** *[43] Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.*

Kila **kila amwaminiye** atapata ondoleo la dhambi ni kwa sababu umemwamini Yesu ndiyo maana umepata ondoleo la dhambi zako. Kuamini maana yake **hauweki matumaini yako katika nguvu zako au jitihada zako bali katika kazi ya Yesu Kristo.** Unaamini ya kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi zako na akafufuka siku ya tatu kwa ushindi. Vyote hivi ni kwa ajili yako. **1 Wakorintho 15:3-*4*** *Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe*, *ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; 4 na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu*, *kama yanenavyo maandiko*.

Alikufa kwa ajili ya dhambi zako na alifufuka ili kukuhakishia kuwa ameshinda dhambi kwa ajili yako. Angalia **1 Wakorintho 15:17** *Na kama Kristo*

*hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu.*

Ujasiri wetu/wako ni katika ufufuo wake.

## UMESAMEHEWA DHAMBI

Biblia inaweka wazi kuwa hakuna mwanadamu anayeweza kujiokoa kutoka kwenye dhambi. Na ndiyo maana Yesu akaja ili apate adhabu yangu na yako. Angalia **Mathayo 1:21** *[21]Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*

Atawaokoa watu wake na dhambi zao, ikiwa ni pamoja na wewe leo.

Hata ungejitahidi vipi usingeweza, angalia **Waefeso 2:8-9** *[8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya*

*imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; [9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.*

Anasema si kwa matendo. Anaongezea hapa **Wagalatia 2:16** *[16] hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki.*

Hakuna mwenye mwili kama mimi na wewe ambao watakuwa na haki mbele za Mungu kwa kujitahidi kuifuata sheria. Ndiyo maana Yesu akaja, akateswa akafa nafasi yangu mimi na wewe. Kumbuka Yeye hakufanya kosa lolote ila amejitwika

dhambi zetu. angalia **2 Wakorinto 5:21** *[21] Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, **ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.***

Tena asema mahali pengine Hii ni sawa na kusema alikaa sehemu ya **ADHABU** yako ili wewe upate **HAKI** yake. Alikubali Mshahara wako wa **MAUTI** ili Akupe **UZIMA WAKE BURE tena zawadi.** Angalia, **Warumi 6:23** *[23] Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.*

Kwa hiyo alikufa ili uwe na uzima wa milele. Angalia hapa **Yohana 3:16** *[16] Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

Kwa hiyo, hautapotea au kuangamia tena. Yesu alishalipia deni la dhambi zako, Fidia imeshalipwa. Kwa hiyo Mungu hazikumbuki wala kuzihesabu dhambi zako. Angalia **Waebrania 8:12** *[12]Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, Na dhambi zao sitazikumbuka tena.* Tena akarudia hapa **Waebrania 10:17** *[17]Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa.*

Kwa sababu Mungu hana tatizo la kusahausahau, hii ina maana gani? Hakumbuki dhambi zako?

Angalia.. **Warumi 4:7-8** *[7] Heri waliosamehewa makosa yao, Na waliositiriwa dhambi zao. [8] Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.*
Amesema hakuhesabii, ina maana hatazileta mezani, amekusitiri. Siyo

dhambi moja, Yesu amekusamehe dhambi zako zote na makossa. **Wakolosai 2:13** *Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe* ***makosa yote.***

Hii ina maana Mungu hatatuhesabia, ametusitiria dhambi zetu. Hakuna siku atatuhukumu, maana Yesu ameshachukua hukumu yangu na yako.

Ndiyo maana sehemu nyingine anasema umewekwa huru mbali na hukumu ya adhabu. **Warumi 8:1** *[1] Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.* Ndiyo maana Paulo aliandika kwenye **Waefeso 1:4** *kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe*

*watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo.* Leo umekaribishwa kwenye familia ya watu wasio na hatia mbele za Mungu.

## KUTOKA KWENYE NGUVU ZA GIZA

Yesu alikufa ili akuokoe na umeokolewa kutoka katika nguvu za giza.

**Wakolosai 1:13** *[13] Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake.*

Uko ndani ya ufalme wa Mungu. Umeitwa kutoka gizani na kuingia nuruni.

**1 Petro 2:9** *[9] Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza*

*fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu;*

Angalia **Wakolosai 1:13** *[13] Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika*

**Yohana 3:5-8** *[5] Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. [6] Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. [7] Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili. [8] Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.*

Mtu hawezi kuingia wala kuona ufalme wa Mungu pasipo kuzaliwa mara ya pili. Wewe umezaliwa mara ya pili.

Hivyo, Mungu amekuokoa kutoka kwenye nguvu za giza na kukuingiza kwenye ufalme wa mwana wa pendo lake. Hivyo, umenunuliwa kutoka kwenye ushawishi wa nguvu za giza. Wewe ndiye mwenye uwezo wa kujizoeza kutumia mamlaka yake dhidi ya nguvu za giza kwa sababu uko juu ya hizo.

**Waefeso 1:21-23** *[21] juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; [22] akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo [23]*

*ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*

Umeitwa kutoka gizani na kuingia katika nuru yake ya ajabu.

**1 Petro 2:9** *[9] Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.*

Uko ndani ya Mungu – Nuru. Uko huru mbali na utawala wa nguvu za giza. Umeketishwa juu sana. Shetani hana mamlaka juu yako tena maana umeweka juu sana kuliko hata alipo.

## UNAWEZA KUWA NA UHAKIKA

Tuanze na maneno ambayo Yesu alisema na wanafunzi wake kabla ya kuteswa. Angalia Yuda pia kwenye **Yuda 1:24** *[24]Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu.*

Anakulinda usijikwae, ndiyo maana hauwezi kuondolewa mkononi mwake. Angalia hili **Yohana 10:28** *Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu*.

Hakuna. Tena anasema **1 Petro 1:23** *Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, linalodumu hata milele.*

Anasema aina ya uzima unaodumu milele unatokana na aina ya mbegu…isiyoharibika. Uzima wa milele hauharibiki kwa sababu mbegu au neno lililokuzaa haliharibiki.

Isaya alitabiri kuhusu uaminifu wa Mungu kwa Sayuni.

**Isaya 49:14-15** *[14] Bali Sayuni alisema, YEHOVA ameniacha, Bwana amenisahau. [15] Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe.*

Mwanamke aweza kusahau lakini Mungu hawezi kukusahau.

Yeremia katika kutoa unabii kuhusu upendo wa Mungu anasema…**Yeremia 31:3** *[3] Bwana alinitokea zamani, akisema, Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu.*

Tazama, ni UPENDO WA MILELE. Huu upendo haujui kupungua, ni wa milele.

Hii ni sababu kwa nini WOKOVU ulioupokea si wa kitambo. Mwandishi wa Waebrania akizungumzia kile Yesu amefanya anasema…**Waebrania 5:9** *[9] naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*

Ni WOKOVU WA MILELE. umepokea wokovu wa milele. Milele maana yake

hauwzi kuchuja. Unadumu milele.

Angalia na **Waebrania 10:14** *[14] Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*

Kwa toleo moja – Kristo, ametukamilisha hata milele. Yesu hatakasi kila siku, amefanya mara moja. Ukiamini unapokea utakaso wake mara moja na matokeo yake ni ya milele. Kwa toleo moja hapa ni kufa kwa Yesu Kristo. Soma **Waebrania 10:1-14.**

## VIPI KAMA NIKITENDA DHAMBI TENA?

Biblia imeshalitazama hivi na kuweka maagizo. Tazama **1 Yohana 2:1-2** *[1] Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi*

*kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, [2] naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote.*

Yohana anaandika kwamba tusitende dhambi. Nia ya Mungu ni kwamba watoto wake wasiwe watenda dhambi. Lakini watoto wanaweza kukosea na hapa anasema tunaye mwombezi kwa Baba, Yeye ndiye upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu amefanya kazi ya kuokoka lakini hata leo anasimama kama mwombezi na kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Shetani atakuletea taarifa ya kukushtaki ili ujione hufai tena mbele za Mungu. Usimsikilize, mwambie hati ya mashtaka yangu Yesu ameiondoa. Angalia **Wakolosai 2:14** *akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu;*

*akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani.*

Angalia na hapa pia, **Warumi 8:31-34** *[31] Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? [32] Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye? [33] Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. [34] Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea.*

Aliyekuwa na uweze peke yake wa kukuhukumu ndiye aliyekufa kwa ajili

yako. Badala ya kukuhukumu anasimama kama mwombezi wako. **Mwombezi** hapa ni neno lenye maana ya *kusimama kama mtetezi wa mwingine.* Maadamu Yesu anaishi hata milele, upo salama ndani yake. Yeye hayupo kinyume nawe bali yupo upande wako daima.

Ukweli ni kwamba unaweza kukosea, lakini makosa hayabadilishi ukweli kwamba wewe ni mwana wa Mungu. Makosa hayakufanyi kuwa mwana wa ibilisi na shetani. Utakuwa mwana wa Mungu aliyekosea. Ni vyema kukaa chini ya mwalimu wa Neno la Mungu au mchungaji akufundishe namna ya kuendelea kuishi maisha ya ushindi kila siku.

## UKUAJI WA UHAKIKA

Kwa kuwa umemwamini Yesu Kristo na amekuwa mwokozi wako, sasa wewe ni mwana wa Mungu, mtakatifu, asiye na hatia mbele zake, umepokea ukombozi wa milele, unao msamaha wa dhambi zako zote. Sasa utajikabidhi katika kuendelea kujifunza ili upate kukua. Ni lazima uwe na mahali ambapo unalishwa neno la Mungu na kuendelea kuimarika ili uwe bora zaidi.

Kwa ajili ya kuendelea kujifunza na kulelewa ili uweze kukua katika kumfahamu Mungu, tumia mawasiliano haya.

**Jina……………………………………….**

**Namba ya simu…………………………**

## Kuhusu Sisi

Huduma ya Global Family Gatherings imejikita katika kufundisha Neno la Mungu kwa uchambuzi wa Maandiko hatua kwa hatua. Nia yetu hasa ni kuishi katika mpango wa Mungu wa kwenda kuhubiri Injili na kutengeneza wanafunzi. Mwisho wa siku tuhakikisha kila mtu, kila mahali amefikiwa na kuimarisha katika kweli ili awe mtu imara na mwenye kutimiza mapenzi ya Mungu hapa duniani.

**Mafundisho kwa njia ya audio**
https://globalfamilygatherings.co.tz/messages/
**Vitabu vyetu nakala tete**
https://globalfamilygatherings.co.tz/our-books/
Makusanyiko simu +255 714 548 565 au
https://globalfamilygatherings.co.tz/about/
utaona maeneo yote yenye makanisa yetu.
Telegram: https://t.me/apostleshemeji
Youtube channel:
https://youtube.com/c/shemejimelayeki
Facebook page:
https://facebook.com/ShemejiMelayeki